


# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

*Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*

WILAYA YA CHEMBA  
FAX/ SIMU 026 2360175  
Barua pepe: [dedChemba@yahoo.com](mailto:dedChemba@yahoo.com)



S.L. P 830  
CHEMBA.

**CDC/LGS/A/5/3**

**27/12/ 2018**

## **TANGAZO LA NAFASI KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kupitia Kibali cha Ajira chenye Kumb.NA.FA.170/360/01/80 cha tarehe 19/12/2018 kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI, anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa kutuma maombi ya kazi zilizoainishwa hapa chini:-

### **1.1. Dereva daraja la II – Nafasi 3**

Sifa za kuajiriwa moja kwa moja:-

- Cheti cha kidato cha nne, Leseni daraja 'E' na 'C' pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari Basic Driving Course yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II.

### **MAJUKUMU**

- (a) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa magari
- (b) Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- (c) Kufanya matengenezo madomadogo ya gari.
- (d) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- (e) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- (f) Kufanya usafi wa gari
- (g) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

Kiwango cha mshahara ;-

TGS B - Tsh. 390,000/= kwa mwezi

### **1.2. Mtendaji wa Kijiji Daraja III– Nafasi 6**

Sifa za kuajiriwa moja kwa moja:-

- (a) Wahitimu wa kidato cha nne na kuendelea waliopata mafunzo ya Taaluma katika fani ya utawala, sheria, maendeleo ya jamii, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Sayansi ya sanaa na Mipango.

## MAJUKUMU

- (a) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Kijiji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika Mipango ya Maendeleo.
  - (b) Atakuwa katibu na mtunza kumbukumbu za vikao vyote vya kijiji.
  - (c) Atakuwa Afisa Mhasibu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Serikali ya Kijiji.
  - (d) Atakuwa Kiongozi wa Watendaji wengine wa Kijiji.
  - (e) Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji
  - (f) Ataratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo za serikali ya kijiji.
  - (g) Atasimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
  - (h) Atafanya kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na mkuu wake wa kazi.
- Kiwango cha mshahara ;-
- TGS B-Tsh390,000/= kwa mwezi

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI


- (a) Barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono.
- (b) Picha 2 (mbili) ndogo za hivi karibuni.
- (c) Wasifu wa mwombaji (CV).
- (d) Vyeti vya kuzaliwa, shule na Taaluma- visibitishwe na Hakimumu ama Wakili, *Results slip na progress Report* hazitakubaliwa.
- (e) Awe na umri chini ya miaka 45.
- (f) Asiwe amewahi kuhukumiwa kifungo jela au kufukuzwa kazi.
- (g) Mwombaji awe tayari kufanya kazi Chemba pasipo kuhama ndani ya miaka mitatu.

## USAILI

Tarehe ya usaili kwa waombaji watakaofanikiwa kufaulu kwenye mchujo (shortlisting) Itatangazwa. Aidha, siku ya usaili mwombaji aje na vyeti halisi vya Elimu na Taaluma. Taarifa ya polisi (Loss Report) kuhusiana na vyeti, result slip havitapokelewa.

Maombi yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, S.L.P 830, Chemba.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 08/01/2019 saa 09:30 Alasiri.



Dr. Semistatus H. Mashimba  
MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)  
CHEMBA